

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 10 Juni, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

SPIKA: Hati za Kuwasilisha Mezani, Waziri Mkuu kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Ummy Nderiananga.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA VIJANA:

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevyta nchini ya mwaka 2021.

SPIKA: Ahsante sana, Katibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 368

Hitaji la Mtaalam wa X-Ray Hospitali ya Wilaya ya Meatu

MHE. MINZA S. MJIKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mtaalam wa *X-Ray* katika Hospitali ya Wilaya ya Meatu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 inaa jiri watumishi 7,612 wa kada mbalimbali za afya, wakiwemo wataalam wa *X-Ray*. Hivyo, Hospitali ya Wilaya ya Meatu itapatiwa mtaalam wa *X-ray* baada ya taratibu za ajira kukamilika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mjika naona amekaa Mheshimiwa...

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Spika, nimesimama.

SPIKA: Mheshimiwa Minza Mjika swali la nyongeza.

MHE. MINZA S. MJIKA: Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru na ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali kweli Waziri amekuwa akinipa ushirikiano sana.

Lakini nilitaka nijue sasa ni lini mtaalam huyo ataletwa kwa sababu tatizo hili limekuwa ni la muda mrefu sana leo Wilaya ya Meatu hospitali ina zaidi ya miaka 30 lakini hatujawahi kupata mtaalam wa kudumu wa *X-ray*, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Minza amekuwa akifuatilia sana sana kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Meatu kupata mtumishi kwa ajili ya huduma za *X-ray* kwenye hospitali ya Meatu na nimuhakikishie kwamba katika ajira hizi ambazo tunakamilisha na mpango ni kuanzia Julai watumishi wetu watapelekwa vituoni tutapeleka mtaalam wa *X-ray* kwenye hospitali hii ya Meatu, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane swalii la nyongeza.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea katika Jimbo la Kilwa Kaskazini na alifika katika hospitali ya Kipatimu na akakuta kuna changamoto kubwa ya mtumishi wa *X-ray* baada ya kuwa *X-ray* ilinunuliwa miaka zaidi ya minne kabla ya mwaka jana ikiwa haitumiki kutokana na kukosa mtumishi wa *X-ray*.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

SPIKA: Swali lako?

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Swali langu ni kwamba mtumishi huyu aliletwa akakaa miezi sita lakini juzi juzi hapa ameondolewa...

SPIKA: Uliza swali.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Nataka kujua je, Serikali ina mpango gani wa kumrejesha yule mtumishi ambaye ameondolewa juzi juzi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tulipeleka mtumishi Hospitali ya Kipatimu lakini kwa sababu za kiutumishi amehamishwa, lakini kwenye ajira hizi ambazo watumishi watapelekwa mwezi Julai tayari ameshapangwa mtumishi wa X-ray kwenye Hospitali ya Kipatimu, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Serikalini mna utaratibu wenu, lakini huu siyo utaratibu mzuri wa mtumishi kuwepo watu wakawa wanapata huduma halafu anaondolewa kabla mtumishi mwingine hajapelekwa hapo. (*Makofii*)

Kwa sababu sasa hapo watu watakuwa wanaenda kuhudumiwa na nani? Mlivyompeleka mwanzo alianza kazi, mnavyomuondoaa mhakikishwe mwingine ameshaenda pale, nadhani ni utaratibu mzuri maadam huduma za afya zimeboreshwa. Mheshimiwa Cecilia Paresso swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na uhaba wa watumishi/wataalam wa hivyo vifaa tiba lakini pia ma-*engineerau* mafundi wa kutengeneza hivyo vifaa tiba pindi inapoharibika inakuwa ni changamoto kubwa sana.

Je, katika ajira zilizoko mnazingatia pia na wataalam hawa ili inapopata *breakdown* yoyote basi inatengenezwa kwa wakati?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresto, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba tumekuwa na changamoto ya upungufu wa wataalam wa vipimo kwa maana *diagnostic issues* ikiwemo *X-ray* na *ultrasound*, lakini Serikali kwanza tumeweka mpango mkakati wa kuwafanyia mafunzo kazini wataalam zaidi ya 300 ambaao watakwenda ku-*cover* mapengo kwenye vituo vya afya na hospitali ambazo zinajengwa ili yale majengo yaliyojengwa na vifaa tiba ambavyo vinakwenda vianze kutumika mapema iwezekanavyo.

Lakini pili tuna wataalam wa ufundi kwa maana ya *biomedical engineers* katika halmashauri zetu na katika ajira hizi pia wataajiri wataalam hao, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Charles Kajege swali la nyongeza.

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Spika, ahsante, vituo vya afya vya Kasaunga, Kisorya na Kasuguti

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

bado havina mashine za *X-ray*; je, ni lini vituo hivi vitapata hizo mashine?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge wa Jimbo la Mwibara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuititia mpango wa UVIKO-19 Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha kwa ajilli ya kununua *digital X-ray* 65 kwa ajili ya halmashauri zetu, lakini kwa sababu tunakwenda kununua kwa utaratibu wa kushirikiana na wenzetu wa *UNICEF* zinaweza zikafika zaidi ya 80, 90.

Kwa hiyo vituo vingi vile ambavyo vinahitaji *X-ray* vitapata, lakini kwa maana ya hospitali za wilaya kama kipaumbele na baadaye tutakuja kwenye vituo hivyo na tuta-consider pia vituo vya Mwibara, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Yustina Rahhi swali la nyongeza.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Spika, na mimi nina swali la nyongeza; hospitali ya halmashauri ya Mji wa Mbulu *X-ray machine* mbovu, kwa hiyo kufanya watu hawa kuhangaika kwenda kwenye vituo vya afya.

Je, Serikali inapeleka lini *X-ray machine* katika Hospitali ya Mji wa Mbulu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Yustina, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika *X-ray* ambazo zitaletwa kipaumbele ni hospitali za halmashauri, kwa hiyo tunachukua hoja ya hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Mbulu ili tuone kama ile *X-ray* haiwezi kufanyakazi basi tuhakikishe katika awamu hii tunapeleka *X-ray*pale wananchi wapate huduma, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mathayo David swalii la nyongeza.

MHE. DKT. MATHAYO D. MATHAYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swalii la nyongeza kwa Jimbo la Same Magharibi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Hedaru na Kituo cha Afya cha Kisiwani, ni vituo ambavyo vinahudumia watu wengi sana lakini vina upungufu wa vifaa tiba. Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba Kituo cha Afya Hedaru na kile cha Kisiwani kinapata vifaa tiba vya kutosha?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo, Mbunge wa Jimbo la Same Magharibi kama ifuatavyo:-

Katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni 69.95 kwa ajili ya kununua vifaa tiba kwenye hospitali za halmashauri zilizokamilika na vituo vya afya viliviyokamilika vya awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama vituo hivi vipo awamu ya kwanza nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kwamba vitapata vifaa tiba lakini kama viko awamu ya pili na ya tatu basi vitapata awamu itakayofuata, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

Na. 369

Mashine ya X-Ray na Ultra Sound kwa ajili ya Kituo cha Afya Makambako

MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. DEO K. SANGA aliuliza:-

Je, ni lini Kituo cha Afya Makambako kitapata mashine ya *X-ray* na *Ultra Sound*?

SPIKA: SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishapeleka mashine ya *X-ray* kwenye Kituo cha Afya Makambako ambayo ilisimikwa kituoni hapo mwezi Machi, 2021 na inatumika.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba 2021 Serikali ilipeleka mashine ya *Ultrasound* katika Kituo cha Afya cha Makambako na inatumika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Hospitali ya Makambako imeshapata *X-ray* na *Ultrasound* naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza; Kituo cha Afya Ikizu kina muda mrefu sana tukiwa na maombi ya *X-ray* na mwaka jana walisema wangepata lakini hawajapata. Ni lini sasa Kituo cha Afya Ikizu kitapata *X-ray*?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo vyetu vya afya vingi havina mashine za *X-ray*, lakini bado tutaangalia vigezo ambavyo vitapelekea baadhi ya vituo kupata kipaumbele kuliko vituo vingine, kwa hiyo, naomba nichukue hiki Kituo cha Afya cha Ikizu ili tukafanye upembuzi na kuona uhitaji wa *X-ray* lakini baada ya hapo tutatafuta *X-ray* kwa ajili ya kituo hicho pia, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dunstan Kitandula swali la nyongeza.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Kituo cha Afya cha Maramba kinachohudumia kata sita Serikali iliahidi kupeleka *X-ray*; ni lini Serikali itapeleka *X-ray*?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Dunstan Kitandula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Maramba ni kweli kwamba kinahudumia kata nyingi na katika mpango ambaao tumeuweka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo hiki pia ni mionganii mwa vituo ambavyo tumepanga kitapelekewa *X-ray*, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa auize swalii lake.

Na. 370

Kujenga, Kusafisha na Kuongeza Kina cha Mto Kanoni Manispaa ya Bukoba

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha kuwa Mto Kanoni uliopo katika Manispaa ya Bukoba unasafishwa, kina kinaongezwa na kingo za mto zinajengwa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshachukua hatua muhimu za kudumu za kuondoa changamoto za Mto Kanoni

ulipo katika Manispaa ya Bukoba. Kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba tayari imeibua mradi wa utunzaji wa Mto Kanoni kuitia mradi wa *TACTIC* unaotarajia kuanza Januari, 2023 wenyewe thamani ya shilingi milioni 500. Lengo la mradi ni kuondoa kero kubwa ya mafuriko ambayo hutokea kila mwaka nyakati za mvua ya masika na kuathiri zaidi ya kaya 331. Mradi huu utahusisha ujenzi wa maeneo makuu mawili ambayo ni kuongeza kina na upana wa mto; na ujenzi wa kingo za mto.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa sasa Serikali imeendelea kuchukua jithada za muda mfupi ambapo Manispaa ya Bukoba kila mwaka hutenga kiasi cha shilingi milioni sita kwa ajili ya shughuli za kusafisha, kupanua na kuongeza kina cha mto kwa kuondoa tope, uchafu na miti.

SPIKA: Mheshimiwa Bernadetha Mushashu swali la nyongeza

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mafuriko katika Mto wa Kanoni ulio katika Manispaa ya Bukoba umewatesa watu kwa miaka mingi na sasa hivi naishukuru Serikali kwa kuweza kukubaliana na ombi la Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba na sasa wanauingiza mto huu katika mradi wa *TACTIC*.

Je, kuna mvua za vuli zitaanza mwaka huu za mwezi Oktoba mpaka Januari; Serikali inaweza ikaongezea fedha kiasi kwenye ile milioni sita inayotengwa na Halmashauri ili kusudi angalau wakafanya ukarabati wa awali isije ikatokea tena mafuriko mwaka huu?

Swali la pili; ili kuweza kuondoa mafuriko kabisa katika mto huu, inabidi mto upanuliwe, kina kiongezwe, kuta zijengwe za mto huu kutoka kwenye Kata ya Kagondo, Rwamishenye, Amgembe, Gireye, Bakoba hadi kuingia

kwenye Ziwa Victoria. Je, katika huu mradi unaokuja wa *TACT/C* haya maeneo yote yatazingatiwa?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la mama yangu Mheshimiwa Mushashu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mama Mushashu kwa sababu katika kumbukumbu yangu ni Mbunge mwana mazingira muda mrefu sana na hili analogumza ni utashi kutoka katika moyo wake kabisa na nikiri wazi kwamba Manispaa imeanza kufanya kazi na Serikali kila muda tunafanyakazi, na Mama Mushashu anakumbuka kuititia mradi wa *UGLSP* pale katika Manispaa ya Bukoba hata mwanzo tulianza kufanya kazi hii kale kamfereji kadogo kalikokuwa kanaenda pale mpaka katika ziwa.

Kwa hiyo, tumetenga milioni sita hata hivyo tutaangalia pale itapobainika kwamba ile milioni sita ina changamoto tutaona nini cha kufanya kwa upande wa Serikali kwa ujumla wake. Lakini katika hizi kata zingine je, zitahusika vipi? Kama nilivyosema ni kwamba lengo letu ni kwamba kuondoa changamoto ya mafuriko na kama ulivyosema kweli katika kata hizi zote zinakabiliwa na mafuriko haya mto unapotokea jambo hili.

Tutaangalia katika ujenzi wa kuta katika mto huu jambo hilo lote litazingatiwa na hata kama kutatakiwa *additional financing* ya kuhakikisha maeneo engine yote tuyaboreshe tutalifanya Mheshimiwa Mbunge bila shaka aina yoyote.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, miliosimama nimewaona, niwakumbushe maswali mafupi na Waziri majibu mafupi, Mheshimiwa Asia Halamga.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi; je, Serikali ina mpango gani wa kuokoa Ziwa Babati kwa kuondoa magugu yanayozidi kukua kwa kasi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la dada yangu Asia, Mbunge wa Manyara Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Ziwa Babati limekuwa na changamoto na magugu sambamba na maeneo mengine. Serikali tumeandaa mpango maalum hivi sasa kubainisha juhudzi tulizonazo juu ya mpango huo lengo kuangalia maeneo ya changamoto mbalimbali. Kwa hiyo, tuko katika stage ya kutafuta fedha siyo Ziwa Babati peke yake lakini na maziwa mengine yanayokabiliana na magugu katika maeneo mbalimbali.

SPIKA: Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Wilaya ya Same Jimbo la Same Mashariki kuna mito mikubwa mitatu ambayo inatitirisha maji bondeni ili wananchi watumie katika umwagiliaji wa mpunga kwenye Kata za Maore, Ndungu na ...

SPIKA: Swali?

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Tatizo hii mito imeja magugu imeja magogo. Je, ...

SPIKA: Swali lako Mheshimiwa Kaboyoka.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Je, Serikali iko tayari kusaidia mito hii isafishwe ili maji yatiririke kwa urahisi? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Serikali kusaidia maeneo mbalimbali na hata eneo hilo kifupi ni kwamba niwatume wataalam wangu kwenda kuangalia kufanya *need assessment* ya eneo lile, lengo ni kwamba tunapoenda kutafuta mipango ya kutafuta fedha na eneo hilo tuweze kulishughulikia maana yake sambamba na Ziwa Jipe ambalo liko katika Wilaya ya Mwanga kule katika Mkoa wa Kilimanjaro.

SPIKA: Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Vijijini swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri.

Mheshimiwa Waziri Jafo ahsante sana kwa majibu yako.

Na. 371

Kuimarisha Jeshi La Zimamoto Maeneo ya Miji

MHE. ZUENA A. BUSHIRI K.n.y. MHE. PRISCUS J. TARIMO
aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kuimarisha Jeshi la Zimamoto hasa katika maeneo ya miji yenye hatari kubwa ya majanga ya moto?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI
aliibu:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika mpango wa kuimarisha huduma za zimamoto na uokoaji nchini kwa kuimarisha na kuongeza vifaa nya kisasa.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 vitajengwa jumla ya vituo saba nya zimamoto na uokoaji kwa kuanza na mikoa isiyokuwa na vituo hivyo. Mikoa hiyo ni pamoja na Songwe, Simiyu, Kagera, Njombe, Manyara, Katavi na Geita.

Aidha, kwa kuzingatia ukuaji wa haraka wa Jiji la Dodoma ambalo ni Makao Makuu ya nchi, ujenzi wa vituo viwili Chamwino na Nzuguni utakamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetua ajira mpya ya askari 400 ambao kwa sasa wapo mafunzoni. Vilevile Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu kinga dhidi ya majanga ya moto kuanzia shulenii, maeneo ya biashara na yale yenye mikusanyiko mikubwa ya watu. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Zueni Athuman Bushiri, swalii la nyongeza.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Naomba niulize swalii; je Serikali haioni haja ya kurejesha huduma hii katika halmashauri sasa hivi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; Wizara imejipanga vipi kudhibiti janga la moto katika masoko nchini? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Bushiri kama kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, moja; kuhusu umuhimu wa kurejesha huduma hizi halmashauri, naomba nilikumbushe Bunge lako tukufu kwamba huko nyuma huduma hizi zilikuwa zinatolewa na halmashauri, baada ya kuthibitika kwamba weledi na uwezo wa halmashauri kutekeleza jambo hili ni changamoto ikaamuriwa huduma hizi zirudi Makao Makuu na ndio ikaimarishwa hili Jeshi la Zimamoto na Ukoaji. Kwa hiyo kama tunazungumza kurejesha itabidi tufanye tathimini kujiridhisha leo ule uwezo ambao haukuwepo miaka kumi iliyopita kama umekuwepo na hivyo kuona umuhimu wa kurejesha hizi huduma.

Hata hivyo, wananchi wanao hudumiwa wapo kwenye halmashauri na wengi ni wafanyabiashara ni wazi kwamba bajeti ya zimamoto ni changamoto, hivyo halmashauri zinatakiwa kuanza kutenga bajeti kwa ajili ya kununua vifaa ili askari wetu walipangwa kwenye maeneo hayo wavitungie vifaa hivyo kuzima moto kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, swali la pili juu ya namna ya kudhibiti majanga ya zimamoto yanayozidi kuongezeka; nakiri kwamba yapo ndio maana nimebainisha mikakati hapa itakayosaidia kuimarisha utoaji wa huduma za zimamoto na ukoaji ikiwa ni pamoja na mafunzo, lakini vilevile elimu kwa umma na kuzingatia weledi katika ujenzi wa majengo yetu. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa changamoto ya vifaa katika Jeshi la Zimamoto ni mtihani hasa katika Manispaa ya Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, unaunguliwa mita 100 zimamoto inakuja inashindwa kuzima moto, je, ni lini...

SPIKA: Swali lako.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaboresha miundombinu ya zimamoto katika Manispaa ya Shinyanga?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ipo mikakati mingi ambayo tunaitumia katika kuboresha, moja; ni ajira kwa kuongeza nguvu kazi lakini pili manunuzi ya vifaa mmetupitishia bajeti hivi juzi zaidi ya bilioni 11 zinakwenda kununua vifaa ambavyo vitapeleka kwenye maeneo yenye changamoto kubwa Ikiwemo Mkoa wa Shinyanga. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Yahaya Massare.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii; kwa kuwa halmashauri nyingi hazina zimamoto, je, Serikali ipo tayari kujipanga upya sasa badala ya kutoka katika sehemu moja za Wilaya na Manispaa na Majiji kwenda katika Halmashauri zetu au kukasimu madaraka ya zimamoto katika Halmashauri ili kuweka wigo mpana wa namna ya kuzima moto katika maeneo yetu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahaya Massare, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema kwenye jibu la msingi zipo halmashauri ambazo hazina kabisa huduma hizo, lakini ipo mikoa pia ambayo haina huduma hizo, ndiyo

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

maana tukasema kulingana na mipango yetu na bajeti tutaanza na mikoa ambayo haina kabisa huduma za zimamoto na ukoaji tukiendelea kuimarisha uwezo huo kwenye mamlaka kubwa kama manispaa, miji na majiji baadaye tutaendelea kupanua huduma hizi kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zipo vijijini. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Spika, ahsante, kutokana na majanga makubwa ya Mkoa wa Dar es Salaam hasa kuunguliwa kwa masoko.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza magari ya zimamoto?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilave, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunatambua kweli kwamba Jiji la Dar es Salaam linaongoza katika majanga haya ambayo tumejiridhisha kwamba mengine ni uzembe, lakini mengine ni miundombinu ambayo husababisha athari za moto.

Kwa kuzingatia hilo ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu tayari tuna magari matatu yaliyokuwa yanatengenezwa na kiwanda chetu cha NYUMBU yatagawiwa kwenye mikoa yenyе changamoto kubwa likiwemo Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mwaka ujao tunayo bajeti ya zaidi ya *Euro* milioni 4.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya magari na maeneo yote yenyе changamoto yatagawiwa vifaa hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swalii dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mkao wetu wa Iringa kuna msitu Mufindi, Mgololo na kuna msitu katika Wilaya ya Kilolo na moto kila wakati umekuwa ukitokea katika hiyo misitu; ni lini Serikali itaona umuhimu wa Wilaya ya Kilolo na Wilaya ya Mufindi kupatiwa gari la zimamoto?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Ritta Kabati swalii lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba maeneo ya Mufindi na Mgololo mara kadhaa hukumbwa na majanga ya moto, niombe tu uongozi wa zimamoto Mkao wa Iringa waweze kupangilia vizuri rasilimali za magari walizonazo ili angalau gari moja liwe kwenye Wilaya ya Mufindi kuwa na ukaribu kwenye maeneo ambayo majanga hutokeea zaidi. Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, sasa aulize swalii lake.

Na. 372

**Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Mkuyuni hadi
Mhandu – Mwanza**

MHE. STANSLAUS S. MABULA aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa barabara ya Mkuyuni hadi Mhandu itatekelezwa?

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*)imeanza kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya Mkuyuni hadi Mhandu ili kujenga kwa kiwango cha lami. Kazi hii ilianza tarehe 6 Juni, 2021 na inatarajiwa kukamilika Julai, 2022. Aidha, baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika, Serikali itatafuta fedha ili kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swalii la nyongeza.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa tayari upembuzi yakinifu unaelekea mwisho na barabara hii kwakweli ni muhimu sana kwa wanachi wa Jimbo la Nyamagana hususani takribani kata tano za Mkuyuni, Mahina, Mhandu pamoja na Butimba; sasa Serikali ipo tayari kuhakikisha kwamba baada tu ya upembuzi yakinifu barabara hii inaanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, pili; barabra hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais; ni lini sasa Serikali itakuwa tayari kuhakikisha ahadi za Mheshimiwa Rais zinatimizwa kwa wakati? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni kweli ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati huo akiwa ni Makamu wa Rais na sasa ni Rais na ndiyo maana barabara hii tayari tumeshaanza kutekeleza ahadi na tayari tunaifanyia usanifu ili iweze kukamilika na tuenze kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, na barabara hii kwa swali lake la pili; tunaipta uzito mkubwa sana kwa sababu ni barabara ambayo tunaamini inakuwa ndiyo barabara kama *bypass* kwa mtu akitokea Nyegezi kwenda Mwanza Mjini ikitokea changamoto yoyote basi hii barabara ndiyo inayoweza kutumika kwa ajili ya kuwapeleka watu katikati ya Mji wa Mwanza. Ahsante.

SPIKA: Oran Njeza swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fursa na mimi ningependa kujua je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Mbalizi - Mkwajuni - Makongorosi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja tayari ipo kwenye ukamilishwaji wa kufanyiwa usanifu wa kina na baada ya hapo Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami ili kuiunganisha Mkao wa Mbeya kwa maana ya Wilaya ya Mbeya na Wilaya ya Songwe kwa Mkao wa Songwe, ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

SPIKA: Mheshimiwa Jackson, swali la nyongeza.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa barabara kutoka Iringa kwenda Pawaga kupita Kihwele - Kalenga ipo kwenye kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi. Je, ni lini sasa Serikali itaweza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara iliyotajwa ipo kwenye llani lakini tu nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatuwezi tukaanza barabara zote kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba kadri tutakavyokuwa tunakwenda basi hii barabara itakuwa ni moja ya barabara ambazo zitajengwa kama zilivyoainishwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020/2025. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Samwelii Hhayuma, swali la nyongeza.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga barabara ya Nangwa - Kisambara - Mkondoa ambayo vinaunganisha Mkoa wa Manyara na Kondoa kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

swali la nyongeza Mheshimiwa Samweli Hhyuma, Mbunge wa Hanang kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni kati ya barabara ambazo zipo kwenye mpango wa kuzijenga kwa kiwango cha lami, lakini ujenzi huo utategemea na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swalii la nyongeza.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii; ahadi ya Mheshimiwa Rais imetolewa pia katika Manispaa ya Kigoma Ujiji ya kujenga barabara ya kilometra 10. Ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa ahadi hiyo ya Rais?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ahadi za Rais zinapewa kipaumbele na Serikali inatafuta fedha ili kukamilisha ahadi hiyo kwa kujenga hizo kilometra 10 ambazo zimeahidiwa na Mheshimiwa Rais, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, swalii la nyongeza.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swalii moja la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais ya kujenga barabara ya Mbuyu wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mjerumani kuptitia Magara hadi Mbulu kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Sillo, Mbunge wa Babati Vijijiini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais ilitolewa wakati anazindua barabara ya Magara na tayari tumeshaanza kufanya usanifu kama alivyoagiza ikiwa ni maandalizi kujenga barabara hiyo ya kutoka Mbuyu wa Mjerumani - Magara hadi Mbulu kwa kiwango cha lami.

SPIKA: Mheshimiwa Hamisi Taletale, swalii la nyongeza.

MHE. HAMISI S. TALETALE: Mheshimiwa Spika, kutokana na ahadi ya Serikali barabara yetu ya Ubena Zomozi - Ngerengere je, lini itaanza kujengwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swalii la nyongeza Mheshimiwa Taletale Mbunge wa Morogoro Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara iliyotajwa imetengewa fedha katika bajeti hii kuianza kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, swalii la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru; Mji wa Bunda uliahidiwa kujengwa kilometra 10

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

barabara za mjini kwa kiwango cha lami ni lini sasa zitajengwa? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swalii la nyongeza Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kusaidiana na Wizara yangu pamoja na TAMISEMI tutahakikisha kwamba ahadi iliyoahidiwa inatimizwa na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kujenga zile kilometra 10 katika Mji wa Bunda. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, sasa aulize swalii lake.

Na. 373

Ujenzi wa Barabara ya Unyoni hadi Maguu

MHE. BENAYA L. KAPINGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Unyoni hadi Maguu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imekamilisha kufungua barabara yote kuanzia Unyoni hadi Maguu yenye urefu wa jumla ya kilometra 25 kwa kiwango cha changarawe. Aidha, jumla ya kilometra 4.22 katika eneo la Mapera zimejengwa kwa kiwango cha lami nyepesi katika sehemu korofii. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kujenga barabara yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini naomba niweke kumbukumbu sawa, barabara hii ina urefu wa zaidi ya kilometra 25, lakini hizo kilometra 25 ndizo ahadi ziko kwenye llani ya CCM kwamba zitajengwa kwa kiwango cha lami na barabara hii ndiyo barabara pekee inayotoa wananchi wa Hagati kuja mjini ni barabara pekee hiyo hiyo tu.

SPIKA: Swali lako.

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, swali langu nimeuliza ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara hii?

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili; barabara hii inaenda mpaka Nyasa, kwa hiyo, kule chini bado hajafunguliwa, je, Serikali iko tayari kuifungua barabara hii hadi kufika Wilaya ya Nyasa? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante na napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbanga Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyo sema kwenye jibu la msingi, barabara hii tunatafuta fedha ili iweze kujengwa yote

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kwa kiwango cha lami, lakini Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba barabara hii inapita kwenye maeneo mengi yenyeye miinuko na makorofin na ndiyo maana Serikali iliona bora ianze kwanza kwa kujenga kwa kiwango cha lami yale maeneo yote ambayo ni korofili ili iendelee kupiditika lakini maeneo mengine yakiwa ya changarawe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuifikisha hii barabara hadi Nyasa naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwakuwa tunaona ni barabara muhimu kuunganisha Mbanga na Nyasa, Wizara yangu kusaidiana na wenzetu wa TAMISEMI - *TARURA* tutakubaliana namna ya kuhakikisha kwamba tunafungua hii barabara hadi Nyasa ili kurahisisha mawasiliano kwa wananchi hawa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, swali la nyongeza.

MHE. NASHON W. BIDYANGUZE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Simbo – Kalya kwa kiwango cha lami? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Simbo – Kalya ipo kwenye llani na Serikali inaendelea kutafuta fedha lakini kabla ya kujenga barabara hii Serikali kwanza imeamua ijenge daraja la kudumu la Mto Malagarasi Chini na hatua ya pili itakayofuata itakuwa ni kutafuta fedha kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

SPIKA: Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, mwaka 1973 Serikali ilifanya uamuzi wa kujenga Kiwanda cha Nguo cha *Mbeya Textile* cha pale Mbeya na lengo lilikuwa ni kwamba kiwanda hicho kitapata malighafi ya pamba kutoka katika Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Mwanza kuitia barabara kutoka Tabora hadi Mbeya.

SPIKA: Swali lako?

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu barabara hiyo haijajengwa hadi leo, kiwanda kile kilikufa. Je, Serikali itajenga lini hiyo barabara kutoka Tabora hadi Mbeya hususan kipande cha kutoka Ipole hadi Rungwa? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda, Mbunge wa Sikunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Ipole - Rungwa hadi Makongolosi ni barabara kuu na ni barabara ambayo ipo kwenye mpango na imetengewa fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, kuanza kwa barabara hii kutategemea tu na fedha itakavyopatikana, lakini tayari ipo kwenye mpango kwa ajili ya kujenga barabara hii. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeona kwenye vyombo vya habari, Serikali imekamilisha mazungumzo na Benki ya Dunia, hivyo kupelekea kupata fedha za ujenzi wa barabara kutoka Mtwara - Mingoyo hadi Masasi kilometa 201. Je, sasa ujenzi huo utaanza lini? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshiniwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Chikota kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais katika jitihada za kufungua nchi na kuboresha usafirishaji, *World Bank* wako tayari kuijenga barabara ya Mingoyo hadi Masasi, barabara kuu ambayo ilikuwa kwa kweli imechakaa. Kuanza kwake kutategemea tu na jinsi taratibu za fedha kuhamisha kutoka *World Bank* kuja kwetu itakavyokuwa zimekamilika, barabara hii itaanza mara moja baada ya kupokea hizo fedha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Francis Mtega, swalii la nyongeza.

MHE. FRANCIS L. MTEGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Rujewa – Madibila – Kinanyambo - Mafinga ni muhimu sana kwa wananchi wa Mbarali na upembuzi yakinifu ulishafanyika; je, ni lini sasa Serikali itaanza rasmi ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Francis, Mbunge wa Mbarali kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, ni kweli hii ni barabara moja muhimu sana na ya kiuchumi na ni fupi kutoka Igawa – Rujewa kuja Mafinga. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa ajili ya kuboresha usafiri katи ya Mbarali na Mafinga, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Henry Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara ya kutoka Masumbwe – Rugunga - Ushirika kwenda kuunganishwa na Mkoa wa Geita, lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maganga, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoainisha itajengwa kadiri fedha zitakavyopatikana kwa kiwango cha lami, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Waziri barabara ya kutoka Chala - Mpalamawe ilikuwa ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano, pia ilikuwepo kwenye llani, lakini sasa hamuitamki. Nataka kujua, mna mpango gani wa kujenga kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni barabara kuu, lakini ni barabara ambayo kwa sababu barabara nyingine ilikuwa inapita kwenye Makao Makuu ya Wilaya, Serikali ili amua kwanza ijenge barabara kupitia Makao Makuu na hii ifuate. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kadri Serikali itakavyopata fedha barabara hii pia itajengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, swalii la nyongeza.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE: Mheshimiwa Spika, ahsante, naulizia barabara ya Kibiti kupitia Dimani kwenda Mloka kwenye Bwawa la Mkakati la Mwalimu Nyerere ni lini itajengwa kiwango cha lami? (*Makoff*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoianisha inakwenda kwenye Bwawa la Nyerere na ni barabara ambazo Wizara inaangalia uwezekano kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ziingie kwenye mpango wa *EPC+F* ili kuweza kuiharakisha kuijenga barabara hii, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mbunge wa Busanda sasa aulize swalii lake.

Hitaji la Umeme wa REA Vijiji vya Jimbo la Busanda

MHE. TUMAINI B. MAGESSA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa *REA* kwenye vijiji zaidi ya 40 Busanda?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Yusuf Makamba, majibu.

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Jimbo la Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Busanda lina jumla ya vijiji 83 ambapo katika vijiji hivyo vijiji 40 vimefikiwa na miundombinu ya umeme na vijiji 43 havina umeme hivyo vimeingizwa katika Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Geita ulikumbwa na changamoto iliyotokana na mkandarasi wa kwanza ambaye ni *M/s Samheung Electric Power Company Limited* aliyeshindza zabuni ya kutekeleza mradi katika Wilaya za Nyang'hwale, Mbogwe na Geita, Mkao wa Geita kushindwa kuwasilisha dhamana ya kutekeleza kazi yaani *performance guarantee* ndani ya siku 28 kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi.

Mheshimiwa Spika, hali hii ilipelekea wakala kuanza upya taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa kutekeleza mradi huu katika Mkao wa Geita ambapo kampuni ya *M/S CRJE-CTCE Consortium* ilishinda zabuni hiyo. *REA* na mkandarasi waliingia mkataba mpya mwezi Januari, 2022 wa kutekeleza mradi huu unaotarajia kukamilika mwezi Julai, 2023. Kwa sasa mkandarasi huyo anaendelea na utekelezaji wa mradi huo

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kwa gharama ya shilingi bilioni 25.4 katika Mkoa wa Geita na Busanda ikiwemo.

SPIKA: Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe, wenyewe maswali ya msingi, ukiwa na swali la nyongeza unasimama kama Mbunge mwininge yeoyote. Ukiwa umekaa, usipoitwa jina, usileté lawama. Leo nawakumbusha kwa mara ya mwisho kuhusu hoja hii.

Mheshimiwa Tumaini Magessa.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali kwamba tunae Mkandarasi *CRE* ambaye anatakiwa kufanya kazi maeneo yetu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali moja ni kwamba nini mpango wa Serikali kuwaunganishia umeme wananchi ambao wamekwishalipia umeme na wamekwishakuwa *surveyed* na wanashubiri umeme huu zaidi ya mwezi mmoja kuunganishiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba taasisi zote kwenye vijiji ambavyo vimeshawekewa umeme zinaunganishiwa umeme ili wananchi na taasisi zile ziweze kutumika vizuri zaidi? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza kwa ufuatiliaji mzuri wa maeneo ya vijiji katika jimbo lake ambayo hayajapatiwa umeme. Kuhusu suala la ambao

wamekwishalipia na hawajaunganishiwa, Serikali imeanzisha programu maalum na kutafuta fedha na kutenga fungu la fedha maalum kwa ajili ya kununua vifaa ambavyo vilikuwa vinakosekana kwa ajili ya kuwaunganishia wateja wote takribani 100,000 ambao hawajaunganishiwa umeme na bahati nzuri kadri siku zinavyoenda tunapunguza hiyo *back log*. Kwa hiyo, kwa wananchi wa Busanda kazi inaendelea na watafungiwa umeme haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu taasisi kama unavyofahamu katika bajeti ya Wizara kwa mwaka ujao wa fedha tumetenga fedha mahususi kwa ajili ya kuunganishia umeme katika taasisi mbalimbali za umma ikiwemo shule na vituo vya afya.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Baadhi ya vijiji kwenye Jimbo la Ukerewe umeme umesogezwa mpaka kwenye transfoma lakini kwa zaidi ya mwaka mmoja umeme huu haujaweza kusambazwa kwenye makazi ya wananchi.

Nataka kujua mpango wa Serikali kuweza kusambaza umeme huu kwenye makazi ya watu. Nashukuru.

SPIKA: Mheshiniwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwa na changamoto hiyo ya kufikisha umeme katika maeneo ambayo watu wanaishi katika Jimbo la Ukerewe na napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zimepangwa, manunuzi yamefanyika ya vifaa vya kuweza kusogeza umeme katika makazi ya watu. Katika mwaka ujao wa fedha tutaongeza kasi ya kuwaunganishia umeme wananchi wa Jimbo la Ukerewe na kote nchini.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Miezi nane sasa au saba, mkandarasi wa *REA* katika Jimbo la Mbulu Mji amesimika nguzo, hajaweka waya wala kuwasha umeme.

Je, ni lini mkandarasi huyo atafunga waya na kuwasha umeme katika Jimbo la Mbulu Mji? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia, Mbunge wa Mbulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulitokea changamoto katika mradi unaoendelea wa *REA* wa kupanda kwa bei za vifaa ikiwemo transfoma na waya ambayo ilipelekeea wakandarasi kuchelewa kukamilisha kazi walizokuwa wamepangiwa kufanya. Bahati nzuri Serikali imekaa na wakandarasi, tumeponga fedha za ziada kufidia gharama zilizoongezeka, tumeingia mikataba mipyä na sasa kazi itaenda kwa kasi zaidi kukamilisha yale maeneo ambayo yalikuwa yamesimama.

SPIKA: Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, ahsante, nataka njue nini kauli ya Serikali kuhusu wananchi kuuziwa nguzo za umeme, kwani mpaka hivi leo kuna wananchi wanataka kuingiza umeme kwenye majumba yao, wanauziwa nguzo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema, Mbunge wa Ulyankulu kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali na Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) hatukubali na haturuhusu watu kuuziwa nguzo katika umeme mkubwa. Pale ambapo ni sehemu ya gharama ya kuunganishiwa umeme inawekwa katika gharama hizo. Lakini pale ambapo Mheshimiwa Mbunge au mwananchi ana taarifa yoyote ya mwananchi kuuziwa nguzo ambapo ni wajibu wa *TANESCO* kuzipeleka, basi atuletee taarifa hiyo na tutashughulika na hilo tatizo haraka iwezekanavyo.

SPIKA: Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, swali la nyongeza.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona; kwa sababu Halmashauri yetu ya Mji wa Makambako ina maeneo ambayo ni vijiji na vitongoji. Je, Wizara haloni sasa ni muda wa kuwapelekea wananchi wa Makambako ambao wanalipa bei za kama mjini wakati mazingira ni vijijini yaliyo mengi? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, na Mheshimiwa Mbunge kama mtakumbuka wakati tunawasilisha bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha tulieleza kwamba tumepokea kilio cha wananchi wengi na Waheshimiwa Wabunge kwamba ni kweli yapo maeneo ambayo yapo katika maeneo ya mijini, lakini yana sifa ya maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, tumeamua tuunde timu ya wataalam kutoka *REA*, *TANESCO* na Wizara ambapo itazunguka kwenye majimbo yote na kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge kukusanya taarifa za maeneo yenye sifa hizo. Baada ya hapo na kwa kweli hatutangoja miezi sita iishe, basi maeneo haya wananchi watalipia gharama za kuunganisha umeme kama wananchi wa vijijini. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Waziri kwenye Kata ya Lupila kuna sekondari na kuna kituo cha afya, umeme *REA III Round Two* haujaweza kufika kwenye eneo lile.

Je, nini kauli ya Serikali kuweza kutuongezea *scope* ya kufika umeme kwenye eneo la taasisi hizi mbili?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali kupeleka umeme na kuweka vipaumbele katika taasisi za umma. Lakini vilevile tunaongea na wenzetu ndani ya Serikali ikiwemo TAMISEMI kwamba pale ambapo kuna ujenzi wa hizi taasisi, basi kupeleka huduma ya umeme iwe sehemu ya gharama ya ujenzi wa hizo taasisi ili kurahisisha kazi ya upelekaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini katika maeneo aliyozungumza Mheshimiwa Sanga ya Kata ya Lupila, naomba nikutane naye kwa mahususi ili tuweze kulifanya jambo hili kwa umahususi wake.

SPIKA: Mheshimiwa Stella Manyanya, swali la nyongeza

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kuwa je, ni kweli bei ya umeme imepanda kwa sababu naona kuna mabishano kwenye mitandao? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Manyanya, Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si kweli kabisa kwamba bei ya umeme imepanda na Serikali inasikitishwa na wale wanaoeneza maneno hayo na uvumi huo kwenye mitandao. Tumeomba mamlaka husika zichukue hatua kwa udanganyifu na upotofu huo unaofanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupandisha bei ya umeme ni mrefu, unahuisha maombi ya *TANESCO* kwa *EWURA* na unahuisha *public hearing* kwamba wananchi lazima wahanishwe na washirikishwe katika kutoa maoni yao pale bei ya umeme inapopandishwa. Ni mchakato mrefu ambao hauwezi kufanya kwa siri.

Kwa hiyo, hizi taarifa kwamba Serikali imepandisha bei ya umeme si kweli na naomba zipuuze na hatua zitachukuliwa kwa wale ambao wanaeneza uvumi huo. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii.

Katika Kata ya Msisima tuna sekondari ambayo inagharamiwa kwa shilingi milioni 600, lakini eneo hilo umeme haujafika. Je, Serikali itakuwa tayari kutupelekea umeme katika eneo la Kata ya Msisima kwenye Sekondari ya Msisima?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha tumepanga fedha mahususi kwa ajili ya kupeleka umeme

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

katika taasisi za umma na bila shaka yoyote Shule ya Sekondari ya Msisima katika Kata ya Msisima na yenyewe itapata umeme katika programu hii.

SPIKA: Mheshimiwa Chaurembo, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itafunga transforma ya *MVA 90* katika Jimbo la Mbagala katika *substation* ya Mbagala?

SPIKA: Mheshimiwa Chaurembo swali linalohusu transforma ni linalofuata. Kwa hiyo, nitakupa nafasi hiyo. Swali hili linahusu umeme wa *REA*.

Mheshimiwa Salome Makamba, swali la nyongeza.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri; katika Jimbo la Shinyanga Mjini hususani Kata ya Kizumbi na Kitangia ambayo kimkakati ni maeneo ya viwanda, umeme haujafika katika maeneo mengi. Nini mkakati wa Serikali kupeleka umeme katika maeneo hayo? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome Makamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba kuna baadhi ya maeneo siyo tu katika Jimbo la Shinyanga Mjini, lakini maeneo mbalimbali nchini ambapo kuna viwanda na ni maeneo ya uzalishaji na umeme haujafika. Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) limeanzisha programu maalum ya kupeleka umeme katika maeneo ya uzalishaji ikiwemo migodi, viwanda na kilimo kwa sababu pia ni maeneo ambayo yanaweza kuipatia mapato Shirika letu la Umeme Tanzania na maeneo haya katika Wilaya ya Shinyanga Mjini pia yatazingatiwa katika mpango huu mahususi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

SPIKA: Mheshimiwa John Marko Sallu Mbunge wa Handeni Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 375

Uhitaji wa Transfoma Mkata

MHE. JOHN M. SALLU aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga kipoza umeme transfoma kutoka kwenye umeme wa msongo wa KV 132 pale Mkata?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa John Marko Sallu, Mbunge wa Handeni Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia bajeti ya Wizara ya Nishati ya mwaka wa fedha wa 2022/2023 imetenga jumla ya shilingi bilioni 16.94 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme chenye uwezo wa MVA 120 kilichopo katika eneo la Mkata, Wilaya ya Handeni Vijijini. Ujenzi wa kituo hicho unatarajia kuanza mwezi Agosti, 2022 na kukamilika mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo hiki utaenda sambamba na ujenzi wa njia ya kusambaza umeme ya msongo wa KV 33 yenye urefu wa kilometra 40 kutoka Mkata hadi Kwamsisi kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa umeme katika machimbo *graphite* yaliyopo katika eneo la Kwamsisi. Pia Mradi huu ni sehemu ya mradi mzima wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Projects*) ambao umetengewa jumla ya shilingi bilioni 500 katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa John Marko Sallu swalii la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

MHE. JOHN M. SALLU: Mheshimiwa Spika, Jimbo letu la Handeni Vijijiini lina vitongoji takribani 770; sasa ni lini Serikali itaona umuhimu wa kupeleka umeme wa *REA* katika vitongoji hususani vile ambavyo vina kaya nyingi? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa John Marko Sallu, Mbunge wa Handeni Vijijiini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza katika Bajeti yetu ya Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha Serikali imeanza program mahususi ya kupeka umeme vitongojini na tumetenga shilingi bilioni 140 kama sehemu ya maandalizi ya kazi hiyo ambayo itaongezeka kasi yake pale ambapo tutakuwa tumeposta rasillimali za kutosha, lakini ni kweli kwamba baada ya kupeleka umeme katika maeneo mengi ya vijijiini, maeneo ambayo yanashibiri umeme ni ya vitongoji na vitongoji hivyo katika Wilaya ya Handeni Vijijiini pia vitazingatiwa katika mipango ya Serikali ya kupeleka umeme vitongojini.

SPIKA: Mheshimiwa Chaurembo swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga transforma yenye uwezo wa *MVA 90* katika *substation* ya Mbagala iliyoko katika Jimbo la Mbagala?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chaurembo, Mbunge wa Mbagala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Jimbo la Mbagala ni moja ya maeneo ambayo yana mahitaji makubwa ya umeme, lakini miundombinu ni finyu, kwa hiyo kumekuwa na changamoto kubwa ambayo Mheshimiwa Mbunge

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

amekuwa anatuletea mara kwa mara, ya kadhia ya kukatika kwa umeme au umeme kuwa na nguvu ndogo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa njema Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Mbagala, kwamba Serikali tayari imekwisha kuagiza transforma hiyo kubwa kwa ajili ya kufungwa katika kituo cha kupoza umeme Mbagala na kabla ya mwaka ujao wa fedha kwisha transforma hiyo itakuwa imefungwa na kuweza kuimarishe upatikanaji wa umeme katika Jimbo la Mbagala, lakini na Majimbo mengine Temeke na mkoa mzima wa Dar es salaam kwa ujumla. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Ndakidemi swali la nyongeza.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa, Kata za Kibosho, Kilima, Kibosho Kat, na Kibosho Magharibi katika Jimbo la Moshi Vijijini lina tatizo la *low voltage*.

Je ni lini Serikali itatusaidia kutatua changamoto hii kwa sababu umeme uwa unawake kuanzia saa tano usiku?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Moshi Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa katika Mkoa wa Kilimanjaro na Wilaya ya Moshi Mjini na Moshi Vijijini kumekuwa na changamoto ya kuffilia kwa umeme na nguvu ndogo ya umeme na Serikali imelibaini hilo na ndio maana imeanzisha programu kubwa kabisa ya *National Grid Stabilization Project*. Na maeneo haya ya Kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge yamo katika miradi ya kuimarishe Gridi ya Taifa. Kwa hiyo, napenda nimpe faraja, na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatekeleza mradi wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kuimarisha upatikanaji wa umeme katika kata zake za Jimbo la Moshi Vijijiini.

SPIKA: Mheshimiwa Isack Kamwelwe swali la nyongeza.

MHE. ENG. ISACK A. KAMWELWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naishukuru Serikali kutenga fedha kujenga umeme wa gridi kutoka Sikonge, Ipole, Inyonga kwenda Mpanda, na ninaishukuru tena kwa kutenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia ya wananchi ambaao mradi huo umemega ardhi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri ni lini sasa utatuma timu yako ili waende wakalipe fidia wale wananchi? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri hilo linaweza kujibisha kama swali la msingi, kwa hivyo utapata nafasi ya kulijibu kama swali la msingi. Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 376

Hitaji la Mahakama ya Wilaya – Momba

MHE. NEEMA G. MWANDABILA aliuliza:-

Je ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Momba na lini huduma za Mahakama za Mwanzo zitaanza kutolewa katika Tarafa ya Msangano?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geophrey Pinda, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA aliibuu:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mombasa ni moja ya Wilaya ambazo zimepewa kipaumbele kwenye Mpango wa ujenzi wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2023/2024 ili kuhakikisha kuwa Mahakama inakuwa na majengo yake yenye na mazuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ujenzi wa Mahakama ya Mwanza ya Tarafa ya Msangano umepangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2022/2023 ikiwa ni pamoja na kufanya maandalizi ya mahitaji kama watumishi ili huduma zitolewe mara baada ya ujenzi kukamilika.

SPIKA: Mheshimiwa Neema Mwandabila swalii la nyongeza.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Katika Wilaya ya Songwe, ujenzi wa Mahakama umeshaanza tangu mwaka jana, je, lini Serikali itamaliza ujenzi katika Wilaya hii? Hilo ni swalii la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini changamoto za Mahakama katika Wilaya ya Ileje ni nydingi sana katika Tarafa zote mbili Mbundali na Ulambia, sasa nilitamani kufahamu ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha katika tarafa hizi zote kutakuwa na majengo ya Mahakama? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katibu na Sheria, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, umalizaji wa jengo la Songwe kimsingi upo mwishoni kabisa, ni matarajio yetu katika muda mfupi ujao jengo lile litaweza kukamilika na kwa sababu ilikuwa kwenye mpango huu unaoishia mwezi wa sita na baada ya kikao hiki cha Bunge tutakwenda kuliangalia ili tujue wapi wamekwamia kwa sababu ilikuwa limalizike haraka.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu Mahakama za lleje, mpango wa Serikali hadi kufikia mwaka 2025 makao makuu yote ya tarafa nchini tutakuwa tumejenga Mahakama ambazo zitakuwa ni bora na nzuri kabisa. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mwandabila baada ya kikao hiki cha Bunge tuwasiliane ili nimpe *detail* ya mpango kazi ambao tumeuweka kwenye suala la ujenzi wa Mahakama zetu, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kwa Serikali na kujibisha.

Waheshimiwa Wabunge mnaotembea na mliosimama mtafute viti vya karibu mkae, ninayo matangazo mengi kidogo, lakini nitaanza na tangazo la wageni walioko hapa Bungeni siku ya leo.

Kwanza ni wageni 20 wa kwangu ambao wamemaliza kidato cha nne Shule ya Sekondari Loleza, Jijini Mbeya mwaka 1994, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 25 ambao ni wanamichezo wa Mbeya City Veterans kutoka Jijini Mbeya, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni hao wakiwa bado wamesimama nadhani mtakumbuka jana miltangaziwa kwamba kutakuwa na mechili ya kirafigi ya mpira wa miguu kati ya Waheshimiwa Wabunge na Mbeya City Veterans Club

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

mechi hiyo itachezwa siku ya Jumamosi tarehe 11 Juni, 2022 saa 10.00 jioni katika viwanja vya *Fountaine Gate Academy* vilivyopo Mlimwa C. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa Tarimba Abbas anawakaribisha sana na amesema huko kutakuwa na zawadi nyingi kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mjitekeze. Ahsanteni sana mnaweza kukaa. (*Makof*)

Kuna maswali hapa nitayajibu baadaye kidogo naulizwa nitakuwa nashabikia timu gani? Nitakuwa nawashabikia Simba na Yanga. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni saba ambao ni Kamati ya Waandaji wa Mbio za *Capital City Evening Run* wakiongozwa na ndugu Nsolo Mlozi, na hawa nao wakiwa wamesimama wanawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba siku ya kesho Jumamosi tarehe 11 Juni, Waheshimiwa Wabunge mnaalikwa kushiriki, mbio zinazojulikana kama *Capital City Evening Run* za umbali wa kilometa tano au kilometa 10, kutegemea na Mbunge atakavyochagua, mbio hizi zitafanyika saa kumi jioni katika Jengo la Kitega Uchumi la Jiji la Dodoma katika Mji wa Serikali Mtumba. (*Makof*)

Washiriki mnatakiwa kufika Mji wa Serikali Mtumba kabla ya saa kumi kwa ajili ya kujisajili na medali mbalimbali zimeandaliwa na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Usafiri wa kuelekea Mtumba Mji wa Serikali ni wa kujitegemea. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kushiriki mbio hizi pia, ahsanteni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anawatangazia kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inawakaribisha katika Maonesho ya Kwanza ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi kwa mwaka 2022 yaliyoanza tarehe 7 Juni na yataendelea hadi tarehe 13 Juni, 2022 katika uwanja wa Jamhuri wa Jijini Dodoma. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Maonesho haya yameandaliwa na Baraza la Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi yaani *NACTEVATE* kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (*TPSF*) na kauli mbiu ya maonesho hayo ni Kuimarisha Ubora na Umuhimu wa Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi kwa uzalishaji nguvu kazi. Wabunge wote mnakaribishwa kuona namna ambavyo wizara imejipanga katika kukuza ujuzi. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, tangazo hili ni la siku ya Jumatatu, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba saa 7.30 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa kutakuwa na semina hiyo ambayo imeandaliwa na Ofisi ya Bunge ambapo mtoa mada atatoka Chuo cha Diplomasia kuelezea masuala mbalimbali ya kidiplomasia na itifaki. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, niwasihhi sana kuhudhuria mafunzo haya, ni ya muhimu sana kwetu sisi kama viongozi, lakini kwetu sisi kama Wabunge. Huko yataongelewa mambo mengi na ninyi mtapata fursa ya kuuliza mambo mengi ikiwa ni pamoja na ukifika pale mezani glasi yako ni ya upande upi, kushoto au kulia ili usiwe unakunywa kinywaji cha mwenzio ukialikwa mahali. (*Makofii*)

Lakini pia yatafundishwa mambo mengi ikiwa ni pamoja na kushika kisu na mkono wa kulia na kushika uma na mkono wa kushoto, kwa hiyo mambo yatakuwa mazuri na pia wanaume kule mtapata mafunzo kwamba ukinunua suti usivae ikiwa ile alama hapa, ile alama inapaswa kuondolewa, ni kwa ajili ya dukani ili usipate tabu kuishusha suti ujue imetengenezwa na nani na size yake pia.

Kwa hiyo hayo yote tutajifunza na inakuwa sio vizuri Mheshimiwa Mbunge si mnamuona jamani Mheshimiwa Waziri Mkuu namna mambo yamekaa vizuri hapo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tuwe tunatazamia tazamia hapo viwango namna hiyo, lakini tukipewa mafunzo itakuwa ni njema zaidi. Kwa hiyo niwaombe sana tujitokeze lakini pia kwa sababu tunapata fursa mbalimbali za kuhudhuria mikutano mingi,

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

lazima ufahamu ni wakati gani unaanzisha wewe, hoja na wakati gani inabidi aanzishe kiongozi mkubwa aliyeo hapa halafu wewe ndio uchangie. Maana wako wengine hajui ye ye kama anatakiwa akikaa pale na Waziri Mkuu hajui kama Waziri Mkuu anatakiwa ye ye ndio aanzishe hoja, anaanzisha ye ye hoja ili Waziri Mkuu achangie. Kwa hiyo, hayo nayo tutajifunza. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe sana tuhuduria, ni mafunzo ya muhimu haya nimeyasema yale madogo madogo, lakini yako mambo makubwa mazito yanayotuhusu sana Waheshimiwa Wabunge. Itakuwa siku ya Jumatatu kwa hivyo, tangazo litarejewa tena ila ni saa 7.30 mchana kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote tuhudurie. (*Makofi*)

Lakini Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge na wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa tunao pia Wanadiplomasia vijana 41 kutoka Taasisi ya Vijana ya Wanadiplomasia ambayo inaongozwa na Ndugu James Magumba, karibuni sana hawa wamekuja kwa ajili ya mafunzo hapa Bungeni, karibuni. (*Makofi*)

Tunao pia wanafunzi 90 na walimu 10 wa Shule ya Sekondari ya *Mvumi Mission* kutoka Dodoma, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wanafunzi 60 na walimu wa tano kutoka Shule ya Sekondari *Peace House* ya Jijini Arusha, karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge, hawa wageni nilosoma nao nimetangaza mwaka makusudi maana kuna watu humu ndani wanasahau kuniamkia. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo ambalo limekuwa likizunguka huko mitandaoni na wengine hata

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Wabunge nao wamepata hizo taarifa na kwa sababu ziko zinatuhusu sisi sote na tungependa kujua uhalisia wa hilo jambo kuhusu Loliondo nadhani wote mmeona hapa na pale, ama kusikia hapa na pale taarifa ikizunguka kana kwamba kuna tatizo fulani hivi huko Loliondo.

Kwa kuwa Serikali ipo hapa Bungeni na sisi kama wawakilishi wa wananchi tunapenda kufahamu uhalisia wa hiyo taarifa inayozunguka, basi nitampa fursa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aseme jambo kuhusu jambo hili kabla hatujaahirisha shughuli za Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania karibu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu unao uhuru wa kusimama hapo au kuja kusema hapa mbele.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nitasimama tu hapa hapa.

SPIKA: Haya ahsante sana.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa ya hali ya Ngorongoro kufikia asubuhi hii baada ya kuwa jana kumekuwa na taarifa inayozunguka kwenye mtandao kuonesha kwamba kuna tatizo kubwa. Kama ambavyo pia Bunge hili tukufu liliwahi kutoa mchango wake juu ya matumizi bora ya eneo la Wilaya ya Ngorongoro lenye maeneo makubwa matatu ya Loliondo, Sare na Ngorongoro, na kama ambavyo Serikali ilitoa ahadi ndani ya Bunge lako tukufu kufanya kazi, kazi hiyo inaendelea na leo hii kazi inaendelea kwa eneo la Loliondo.

Mheshimiwa Spika, nini kinaendelea? Baada ya kuwa Serikali imechukua jukumu hilo, tulianza na elimu ya namna bora ya matumizi ya maeneo yale. Tumefanya mikutano Loliondo na Ngorongoro, tumefanya mikutano na wadau kwa lengo la kuwaelimisha nini Serikali inafikiria katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kuboresha matumizi ya uhifadhi kwenye eneo hilo na hasa ilikuwa ni kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kukutana na wananchi wanaoishi maeneo hayo, kushauriana namna bora ya kuhifadhi na kwamba maeneo hayo yawe endelevu. Na Mheshimiwa Rais alisisitiza kukutana na kuzungumza na zoezi hilo limefanyika na linaendelea kufanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika na Watanzania wote ambaو wanatusikiliza kupitia kipindi hiki, Wilaya ya Ngorongoro ina maeneo haya matatu yenye shughuli tofauti. Pale Loliondo tuna eneo ambalo ni mapito ya wanyama, lakini eneo hilo hilo ndiyo mazalia ya wanyama ambaو wanakwenda mpaka kwenye Mbuga ya Serengeti na kupandisha mpaka nchini Kenya na kurudi tena.

Kwa hiyo, wanatengeneza mzunguko kila mwaka ambaو pia unafanya utalii kwenye nchi hizi mbili kuwa kivutio kikubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini eneo hilo hilo pia ni chanzo cha maji, maji ambayo yanatiririka kutoka kwenye chanzo hicho kilichopo Loliondo kinapita Ngorongoro na hatimaye kukamilisha Mto wa Maasai Mara kwenda nchini Kenya na kurudi tena kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, Loliondo ni mahali muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo hili liko karibu na vijiji 14 vilivyoko Wilaya ya Ngorongoro kwenye eneo la Loliondo ambavyo viko mbali sana, kijiji cha karibu sana kiko kilometa nane kutoka katikati ya kijiji mpaka kwenye eneo hilo la mazalia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa tunatoa elimu tuliwaambia tunatambua kwamba wananchi wa eneo hili la Loliondo katika vijiji hivi 14 wanalitumia kwa ajili ya malisho na kunyweshea maji, lakini pia eneo hili ndiyo chanzo cha maji, eneo la mazalia na ndilo pia eneo hili linalozungukwa na hawa wanyama na kutengeneza mzunguko wa wanyama ambaو leo hii ni kivutio kwa utalii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua kuwa eneo hili ni muhimu tuliwahakikishia wananchi kwamba tutaandaa mfumo wa matumizi bora wa pamoja katika wananchi wa vijiji vyote 14 pamoja na Serikali, na tumefanya vikao na Madiwani, na viongozi wa kimila, tumefanya hivi vikao pia na akina mama peke yao ili kuwaondolea usumbufu ambao unatokana na upotoshaji unaofanywa na baadhi ya watu wasiopenda maendeleo ya nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunatambua ziko taasisi tumezisajili ambazo zinajishughulisha na uhifadhi, lakini katika hili inaonekana mara nyingi kazi yao wao ni kupotosha na kuchonganisha katika raia wanaokaa kwenye eneo lile ambao ni wafugaji na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa tumetoa elimu ya matumizi ya eneo lile, tuliamua (Serikali), tuweke alama kwenye eneo lile ili liweze kutambulika na wenyeji wanaoishi pale pamoja na Serikali. Alama hizi siyo wigo, lakini ni alama inayoonesha kwamba unapofika hapa kama unataka kulisha, ukifika huku ni kwenye chanzo cha maji. Na kwa kuwa tutatumia eneo hili kwa mpango wa pamoja katika Serikali na wao, tuliamini alama hizi zitatusaidia sote; watumiaji pamoja na Serikali katika kulilinda na kulihifadhi eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunajua bado kuna watu hawapendi zoezi hilo, lakini wako ambao wanaoelewa, wale wasiopenda ni pamoja na wale wachonganishi ambao wanababisha mtafaruku kwenye mpango mzima wa Serikali wa kuhifadhi eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuweka zile alama limeanza juzi, kama nilivyosema eneo hili linalowekwa alama liki mbali sana na makazi ya watu. Na kwa eneo la Loliondo, zoezi hili halitawezesha kuondoka mtu ye yote anayeishi kwenye eneo lile. Vijiji vitaendelea kubaki kama vijiji, shughuli za wananchi zitaendelea kuwepo na eneo lile tutaendelea kulitunza sote; wanavijiji vile 14 pamoja na Serikali. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa tunapitisha magari kwenda huko msituni, Kijiji cha Lulosokwan ambacho ndicho kilichopo karibu lakini kwa umbali wa kilometra zaidi ya nane mpaka tisa, hawa jana walikutana mahali wakawaita viongozi wao wakaja kuelezana, sasa unapokutana kwenye kundi kama hili kunakuwa na wale wanaopenda na wasiopenda.

Kwa hiyo wakaanza kutengeneza *video* na wale waliokuwa wanahamasisha ili kuonesha kwamba kuna tatizo huko, lakini hakukuwa na kundi lolote, ama la askari ambalo lilikuwa linataka kufanya kitendo chochote kibaya dhidi yao, walikuwa wao wenyewe tu wakiwa wanafanya majaribio, yaani kama vile wanatishia ili wapige picha wazirushe ionekane kwamba Loliondo kuna tatizo. Na ndiyo sababu *video* ile huoni kama kuna askari yejote ambaye anatishiwa mishale. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hali hiyo, Mkuu wa Wilaya na Kamati ya Ulinzi ya Wilaya ya Ngorongoro iliwhaitaji viongozi wa eneo lile, Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Viongozi wa Kimila, ili kuwaambia kwamba lile zoezi sasa ndiyo linaanza na hawa wanapita tu wanakwenda huko misituni kwa ajili ya kuweka zile alama (*beacons*). Baada ya hiyo wale viongozi walirudi, walielimisha na wananchi wao, lakini bado viongozi wale walikwenda wilayani kwa ajili ya mazungumzo zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo *video* iliyorushwa ilikuwa ni mkakati wa kutengeneza tui li kuleta *image* mbaya ndani na nje ya nchi. Lakini kimsingi hakuna mapambano yoyote, hakuna askari aliyekwenda huko kijiji ni kwenda kutishia kwa namna yoyote ile kwa sababu kwenye mipango yote hakuna kijiji kinaondolewa, hakuna mwananchi anaondoka, hakuna tatizo lolote la mifugo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuliona tuseme hili ili kuwaondolea Watanzania dhana mbovu dhidi ya Serikali kwamba labda Serikali inataka kuwaondoa hawa wafugaji, inataka kuvunja vijiji vya wafugaji, hasa vijiji hivyo 14 kwenye eneo la Loliondo.

Baada ya kazi hiyo kukamilika, sasa Serikali itakaa pamoja na viongozi na viongozi wa kimila na wananchi, kuandaa mfumo bora wa matumizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajua eneo lile ndilo linalotumika kwa kulisha na kunywesha maji. Nini Serikali inafanya; Serikali sasa inajenga visima nya maji na Wizara ya Maji iko *site* wanachimba visima na maji yameanza kupatikana. Lakini pia tumepeleka Wizara ya Mifugo kwenda kujenga majosho na kujenga mabakuli ya kunyweshea mifugo ili kuondoa tatizo la unyweshaji maji mifugo tulio nayo kwenye vijiji vile 14 au vijiji nya jirani ya vile vijiji 14 vilivyopo maeneo ya Loliondo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la malisho najua bado ni gumu kwa sababu hali ya hewa siyo nzuri sana, lakini hata hivyo, tumekubaliana kwamba upo utaratibu tutauweka pamoja na hasa inajitokeza kipindi cha Julai, Agosti, Septemba mpaka Oktoba. Kipindi hiki tutaweza kuzungumza pamoja na kuratibu utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Watanzania na wana Loliondo wanansikia; lile eneo kama tutatumia mifugo ya Watanzania tu linaweza kuratibiwa vizuri zaidi na itakuwa mchango endelevu, lakini tukiruhusu kuongeza idadi ya ng'ombe kutoka pengine popote pale eneo hilo litapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba wale wote ambao wanawahamasisha vibaya wananchi wale wataacha mara moja kufanya hivyo ili kuwafanya wananchi wale kuendelea na shughuli zao bila ya kupoteza amani. Tunajua hawa wapotoshaji wanawasababishia akina mama kupata usumbufu, watoto wadogo wanapata usumbufu, lakini wazee wanapata usumbufu bila sababu yoyote ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niwaambie Serikali iko macho dhidi yao, hatutamuonea mtu yejote, na kwa hiyo wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro, eneo la Loliondo

watulie, hakuna shughuli yoyote ya kumhamisha mtu, hatuna lengo la kumhamisha mtu. Eneo lile ni letu sote na tutaliratibu vizuri baada ya kuweka hizo alama ambazo tunataka kuashiria tu kwamba huku ndani ndiko kule ambako tumeatifadhi na tunaratibu vizuri, tunaweza kuratibu kwa pamoja. Hayo ndiyo malengo ya Serikali kwa eneo la Loliondo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Sare. Sare inakaliwa na wafugaji na pia eneo lile linatumika kwa kilimo, lina rutuba nzuri; eneo hili halina tatizo lolote lile. Tunaendelea na shughuli za kawaida na wananchi wanaendelea na shughuli za kawaida.

Mheshimiwa Spika, sasa Ngorongoro huku nako kuna shughuli zake tofauti. Tumefanya vikao na wananchi, tumefanya vikao na vlongozi; Madlwani, watendaji wa kata, watendaji wa vijiji, viongozi wa kimila, lakini tumekutana pia na wadau wa eneo lile kwa ajili ya kutoa elimu na tumefanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Spika, kimsingi eneo lile idadi ya ng'ombe na mifugo kwa ujumla wake imeongezeka sana, idadi ya nyumba zilizojengwa kiholela imeongezeka sana, lakini pia idadi ya watu nayo imeongezeka sana na idadi hii tukiacha ikaendelea bila kwenda kutoa elimu na kushirikiana kusaldia kupunguza kiwango cha idadi ya watu, mifugo na nyumba, suala la utalii katika eneo hilo litakuwa ndoto kwa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo vikao vyote tulivyoviendesha tulikuwa tunajadiliana namna bora ya kupunguza idadi ya watu, kupunguza idadi ya mifugo, kupunguza ujenzi holela wa nyumba na makazi mengine; vikao vyote, na vikao hivi vimeshirikisha wananchi mpaka wao wakasema tunaomba tukuletee maoni yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na mimi niliwapa fursa ya kutengeneza maoni yao, nimewapa mwezi mzima, na wiki moja iliyopita walikuwa hapa viongozi wawakilishi 60 walikuja

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

hana. Na mimi nimekutana nao saa nne usiku pale juu.
(Makofi)

Viongozi wale 60 ni wawakilishi; Mbunge alikuwepo, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Ngorongoro alikuwepo, wazee maarufu walikuwepo, viongozi wa kimila walikuwepo, Madiwani walikuwepo, wawakilishi wa akina mama walikuwepo, wawakilishi wa vijana walikuwepo na wawakilishi wa wazee nao walikuwepo. *(Makofi)*

Nimewakaribisha, nimepokea maoni na sasa yanafanyiwa kazi, maoni haya ya namna bora ya kupunguza watu, mifugo na ujenzi holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tulipokuwa tunatoa elimu, sisi tulitoa fursa tukiwa tunasubiri utekelezwaji wa maoni haya tukasema, wale ambao wako tayari kuhama wenyewe kwa hiari yao wajjandikisha kwa sababu Serikali tunayo fursa ya eneo la kuendesha shughuli za mifugo l'ililopo Wilayani Handeni, Mkoani Tanga, eneo la Msomela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zoezi hilo kwa walioridhia, wameshaanza na taarifa mpaka jana jioni kaya 293 zimejiandikisha, wenyewe kwa hiari yao. Kaya hizi 293 zenye watu 1,497 wamejiandikisha kwa hiari yao. Idadi hii ya watu tunaipeleka Kijiji cha Msomela, Wilayani Handeni, Mkoani Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatujaanza bado kwa sababu Serikali ilikuwa inajipanga vizuri kuandaa mazingira mazuri ya wao kwenda kuishi. Mazingira hayo ni pamoja na ujenzi wa nyumba, mpaka leo hii tumeshajenga nyumba 103 na zimekamilika kwa asilimia 100 na kila nyumba iko kwenye eneo la heka tatu, eneo ambalo linamwezesha mkazi huyu kufanya shughuli nyingine, hata kuweka boma la kuweka mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wananchi hawa pia tumewatengea eneo la malisho ambalo wataendesha shughuli zao za malisho, atatoka pale nyumbani anakwenda kwenye malisho, maeneo mazuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa tumewajengea majosho na maeneo ya kunyweshea maji, kazi inaendelea. Kwenye kijiji kile tumechimba visima mpaka leo tuna visima vitatu vinatoa maji ya kutosha kwenye eneo lile na kijiji cha jirani. Lakini wananchi hawa wakienda huko Msomela wakitaka kulima tumewatengea na eneo la kilimo, fursa ambayo haipo kule Ngorongoro. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Watanzania, kule Ngorongoro hakuna mtu anayeruhusiwa kujenga nyumba ya kudumu, hakuna mtu anaruhusiwa kuendesha kilimo, hakuna mtu anaruhusiwa kufanya biashara. Hawa ni Watanzania wenzetu, tumeamua kuwapa fursa hizo. Tumewajengea nyumba nzuri yenyeye vyumba vitatu iliyopo kwenye eneo la heka tatu, tumewatengea maeneo ya malisho ya wazi kabisa, tumewatengea maeneo ya kilimo ili waweze kulima chakula chochote kile. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika na ndugu Watanzania, hatujaishia hapo, tumeshajenga shule ya msingi yenyeye vyumba saba, tumejenga sekondari yenyeye vyumba vinane na shule zote zimekamilika, tumekarabati zahanati ambayo sasa itakuwa inatibu wagonjwa wa kutoka kijiji kile na kijiji jirani ambachcho pia na chenyewe wanakaa wafugaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI sasa kwenye kata ile tunalazimika kujenga kituo cha afya kwa sababu jamii inayokuja ni kubwa na pana ya watu wengi ili tuwe na kituo cha afya eneo hilo. (*Makof!*)

Sasa Watanzania wenzangu, sasa Serikali inafanya haya yote, tunataka nini tena? Watanzania wenzetu hawa wafugaji ambao wanatoka eneo la Ngorongoro waliojiandikisha wenyewe kwa hiari yao, wako tayari kuhama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tumefanya tathmini ya nyumba zao, siku tutakapoanza zoezi la kuwaondoa tutapeleka mabasi kwa ajili ya kuwasafirisha, tutapeleka lori kwa ajili ya kubebea *furniture*, tutapeleka malori kwa ajili ya kubebea mifugo na tunawalipa fidia ya nyumba zao. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, maandalizi yote haya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameshatoa fedha, fedha tunayo, sasa kazi iliyobaki ni kwenda kutekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huu ni utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kwamba nendeni mkakae nao, mzungumze nao na hatimaye muone namna bora ya kupunguza idadi ya watu, mifugo na ujenzi holela wa nyumba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nani ameumia katika hili? Wapi tumevunja nyumba? Nani anahamishwa kwa nguvu? Kwa nini wapotoshaji wanaingia hapa na kufanya haya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika na Watanzania ambao wanatusikiliza, ndugu zetu hawa ambao wanakwenda Msomela wakishapata zile nyumba zao wanapewa na hati ya nyumba zao na kati ya wote ambao wamefanyiwa tathmini na wanakwenda pale, 173 wameshapigwa picha tayari kwa hati na picha zitaendelea kupigwa kwa wale wote waliofanyiwa tathmini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mpaka tunafikia hatua hii tumeshafanya tathmini ya idadi ya watoto ambao wataanza chekechea 250, watakaoingia shule ya msingi 181 na wanafunzi wa sekondari wako 36. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na tunapofanya haya, nataka niwaambie Watanzania, zoezi hili siyo endelevu na maeneo mengine, hili ni kwa ajili ya Ngorongoro tu. Nimeona nitamke hili wazi isije ikajenga mazoea na maeneo mengine kutaka wajengewe nyumba, hili ni kwa ajili ya Ngorongoro tu na ni kwa sababu maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nirudie tena, Serikali yenu Watanzania, inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ina nia njema na Watanzania, na katika hili linaloendelea Ngorongoro la kufanya maboresho ya maeneo haya ambayo pia yanatoa mchango mkubwa wa utalii

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

nchini na kupata mapato, tutaliendesha kwa namna ambayo hakuna yeyote atakayepata madhara katika hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nataka nirudie tena kwamba kilichotoka jana siyo uhalisia, ni watu walismama wanalenga mishale, lakini hakuna anayemlenga, katika ile *clip* anamlenga nani? Hakuna askari wamekwenda vijiji, hakuna. Hakuna askari amemuuliza mtu yeyote, hakuna. Hakuna tishio lolote zaidi ya kwamba wale wamekwenda kule msituni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena, kwamba eneo hilo liko mbali sana na vijiji, kijiji cha jirani ni kilometra nane. Ni vile wenzetu vijiji vyao vimekaa kama barabara, vinaanza huku vinakwenda mpaka mpakani na Serengeti. Kwa hiyo, inawezekana eneo lile liko sehemu ya kijiji lakini ni mbali mno, na vijiji pekee vya utaratibu huo, kote huku hatuna vijiji vya utaratibu huo wa zaidi ya kilometra tisa, kumi kutoka katikati ya mji.

Mheshimiwa Spika, lakini bado tumesema tutaendesha zoezi hili kwa utulivu na amani na wananchi wa Loliondo waendelee na shughuli zao, wasiwe na matatizo yoyote yale wala wasihofu na mtu yeyote atakayepotosha wala asisikilizwe, wasikilize nini Serikali yao inasema. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika na Bunge lako tukufu, kwa hiyo niliona ni muhimu haya tukayaeleza kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania ambao wanatusikiliza ili waweze kuona nia njema ya Serikali yetu katika kuratibu shughuli za uhifadhi nchini na kwa eneo la Ngorongoro. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na mimi nataka nirudie tena kusema, na nilishawaambia mara nydingi, wamefanya kazi nzuri kwa miaka mingi kwa kuhifadhi eneo hilo na kufikia hatua hiyo, lakini sasa tumegundua iko hatari ya shughuli za uhifadhi kupotea tukiachcha ongezeko lile la watu, ongezeko la mifugo na ujenzi holela wa maeneo yale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, maoni yao waliyoyleta yanaendelea kufanyiwa kazi. Tutakuwa na kikao kingine cha kuitia maoni, tutashirkiana wakati wote ili tufikie hatua nzuri na ilio endelevu katika kuhifadhi eneo letu la Ngorongoro likianzia kule Loliondo mpaka Ngorongoro na kuingia Serengeti ambako sasa kuitia filamu ya *Royal Tour* ambayo pia imeibua walio wengi ambao hawakuwa wanajua Tanzania ina fursa gani wanaanza kuja likiwemo na eneo hilo. Taarifa nzuri tunazo, hata zilizoko huko hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, na leo Mji wa Karatu uliopo Wilaya ya Karatu umeingia kwenye fursa ya kupokea wageni wengi mpaka Mto wa Mbu. Kwa hiyo, shughuli za kiuchumi zimeongezeka. Na hii ndiyo fursa ambayo Mheshimiwa Rais alikusudia alipokuwa anatengeneza filamu yake ya *Royal Tour*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliona nitoe taarifa hii na Waziri wa Maliasili na Utalii na timu yake pamoja na Makatibu Wakuu wako huko katika kusimamia haya, uongozi wa Mkoa wa Arusha uko huko kusimamia haya, kwamba utulivu na kila kitu kinaendelea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nihitimishe kwa kueleza hayo, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru kwa maelezo hayo uliyoyatoa ya kina kabisa. Lakini sasa kwa hawa ambao mnaendelea na mazungumzo sisi tunawapongeza na tunawatakia kila la heri, tunaamini yataisha salama na yataisha vizuri kwa maana ya uhifadhi, lakini pia wananchi wawe salama. (*Makofi*)

Ila tunatamani tuanze kuona hatua zikichukuliwa dhidi ya hawa wanaofanya upotoshaji. Kwa sababu upotoshaji umeanza muda kidogo na Serikali imekuwa ikifafanua na kwenda huko kwenye ziara, ikitoa habari, ikifanya hiki na kile. Lakini jambo hili nafikiri linaendelea kwa sababu hakuna hatua zinazochukuliwa dhidi ya wale wanaofanya hasa wale walioko hapa nchini. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kwa sababu sisi Wabunge tunafahamu na Serikali inafahamu kwamba hata wananchi wengine wanaotaka kufahamu pia wanafahamu kwamba tuko kwenye vita ya kiuchumi na nchi nyingine. Sasa tukiwaacha hawa wakaendelea kutumika wale walioko hapa nchini sheria zetu zichukue mkondo wake. (*Makofii*)

Kama mtu anafanya upotoshaji kama huyo ambaye amechukua hiyo *clip* na inajulikana ameichukulia wapi, tunaweza kuanza na huyo halafu wengine watakuwa wanafuata ikiwa ni pamoja na hizi taasisi ambazo zimesajiliwa hapa nchini kwetu tukifikiri kwamba zina lengo jema na sisi hapa nchini. Lakini kama zinafanya jambo tofauti pia sheria zichukue mkondo wake. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi tunakushukuru lakini tunatamani hata kama ni sehemu ya mazungumzo, lakini mngeanza naye huyu ambaye amezua hii tataruki, halafu wengine watafuata kadri wanavyojitokeza. Na ninaamini hawatakuwepo tena wanaojitokeza kufanya huo upotoshaji kwa sababu watajua kwamba Serikali inafuatilia na hawatakuwa wanaleta tena hayo mambo ambayo hayapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nadhani hili litatusaidia sana hasa kipindi hiki ambacho wewe mwenyewe kama ulivyosema kwamba tunazungumzia *Royal Tourna* tunaamini mambo yatakuwa mazuri zaidi.

Kwa hiyo, hatutaki watu waanze kuzuiwa huko na *clips* za namna hii kuja Tanzania wakijua kwamba naweza kwenda huko nikapigwa mshale au naweza kwenda huko nikakutana na jambo fulani. (*Makofii*)

Sasa tukianza kuchukua hatua itatusaidia sana kuunga mkono juhudii za Mheshimiwa Rais za kuhakikisha sekta yetu ya utalii inakuwa na yejote anayetuzuia katika juhudii hizo za kuhakikisha sekta hii inakua basi Serikali ichukue hatua. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 13 Juni, saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 4.20 Asubuhi, Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 13 Juni, 2022, Saa Tatu Asubuhi)